**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA KAKONKO**

SHULE YA SEKONDARI KAKONKO WASICHANA,
S.L.P. 03,
**KAKONKO.**

Simu Na.
Mkuu wa Shule : 0765768150
Makamu Mkuu wa Shule : 0765992528

Mzazi/Mlezi wa ………………………………..

TAREHE ………………………..

**Kumb, Na.KGSS**/AI/JI/27/05/2026.

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KAKONKO WASICHANA KIDATO CHA TANO, HALMASHAURI YA WILAYA YA KAKONKO MWAKA …………**

**1.0. Utangulizi.**

Ninafurahi kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika Shule ya Sekondari Kakonko Wasichana mwaka ……………, Hongera sana. Muhula wa kwanza wa masomo utaanza tarehe ……………**,** kwa hiyo unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia **tarehe …………** na mwisho wa kuripoti ni **tarehe ……………………...**

Shule ipo kijijini Kanyonza, Katani Kanyonza katika Halmashauri ya Wilaya ya Kakonko, mkoa wa Kigoma (Barabara ya Kakonko - Nyakanazi) kilometa 8 kutokea stendi kuu ya Mabasi - Kakonko.

Usafiri wa bodaboda kutokea kituo cha mabasi Kakonko ni shilingi 4000/=, na kwa Magari madogo shilingi 2000/=

**2.0. MAVAZI**

**2.1. SARE ZA SHULE**

a) Sketi mbili rangi ya kijivu draft yenye urefu hadi chini ya magoti (lindabox), kwa anayehitaji kununua shuleni inapatikana kwa kiasi cha **shilingi 20,000/= kwa kila moja**

b) Shati mbili nyeupe zenye mikono mirefu zisizo na mapambo yoyote wala zisibane aje nazo.

c) T-shirt za shule mbili za rangi ya kijivu iliyokolea zenye kola na Nembo ya shule kwa anayehitaji kununua shuleni inapatikana kwa kiasi cha **shilingi 15,000/= kwa kila moja.**

d) Sketi rangi ya kijani jeshi kwa ajili ya kushindia kwa anayehitaji kununua shuleni inapatikana kwa kiasi cha shilingi **20000/= kila moja.**

.

e) Soksi nyeupe jozi mbili aje nazo.

f). Viatu pea mbili vyeusi vya ngozi vinavyofunika miguu vyenye kamba na visigino vifupi aje navyo.

g). Sweta rangi ya kijani jeshi kwa anayehitaji kununua shuleni inapatikana kwa kiasi cha **shilingi 15,000/=**

h) **Kwa waislam wanaruhusiwa kuvaa juba nyeupe darasani na ya rangi ya kijivu kama vazi la kushindia, zishonwe kwa kufuata maelekezo ya serikali**.

## 2.**2. SARE ZA MICHEZO**

a) Raba za michezo kwa wanafunzi wote aje nazo.
b) Track suit kwa wanafunzi wote rangi ya kijivu iliyokolea yenye michirizi myeupe aje nayo akiwa amevaa kama inavyoonekana kwenye picha



**NB: MWANAFUNZI HARUHUSIWI KUJA NA NGUO ZA NYUMBANI.**

## 3.0. VIFAA VYA SHULE

### 3.1. VIFAA VYA TAALUMA

Kila mwanafunzi anashauriwa kuwa na vifaa vya taaluma vifuatavyo:-

(i) Daftari kubwa kumi (10) kaunta books Quire three,
(ii) Mkebe wa Hisabati (Mathematical Instrument set),
(iii) Kamusi ya kiingereza kwa kiingereza,
(iv) **Mathematical Table ya baraza** la mitihani (uandike jina lako katika kitabu,

(v) Rula, kalamu za wino na penseli,
(vi) Begi la kubebea madaftari, na vifaa vya darasani,
(vii) Aje na tochi ya betri au taa ya sola endapo umeme utakata itumike kwa dharura,
(viii) Rimu mbili (2) A4 “double A” kwa mwaka,
(ix) Aje na Scientific calculator, na
(x) Aje na vitabu vya tahasusi husika vilivyoidhinishwa na taasisi ya elimu (TIE).

### 3.2. VIFAA KWA AJILI YA MATUMIZI BINAFSI

i. Mwanafunzi aje na godoro la futi $2^1/_2$ x6,
ii. Mashuka mawili ya rangi ya **pink,**
iii. Mchango wa **BIMA YA AFYA CHF Tsh 5000/-** au kama anayo aje nayo **BIMA YA NHIF**,
iv. Mfagio wa mti mrefu mmoja,
v. ndoo mbili za lita kumi,
vi. Dumu la lita tano la kutunzia maji ya kunywa,
vii. Beseni la kufulia, fyekeo, jembe vyote vipya,
viii. Kila mwanafunzi aje na Tranka imara la kutunzia vifaa vyake lenye kufuli imara,
ix. Kila mwanafunzi aje na vyombo vya chakula yaani sahani moja, bakuli moja , kikombe na kijiko kimoja,
x. Aje na chandarua rangi nyeupe,
xi. Blanketi nzito,
xii. Aje na taulo la kujifutia baada ya kuoga na taulo za kike.

## 4.0 SHERIA ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa Sheria Na 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya Elimu nchini na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu. Kila mwanafunzi analazimika kuwa na nidhamu ya hali ya juu katika Maongezi na walezi wake pasipo kutumia lugha chafu, hivyo unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo kwa umakini mkubwa sana.

### 4.1. MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUSIMAMISHWA MASOMO AU KUFUKUZWA SHULE.

i. Wizi,
ii. Uasherati, ushoga na ubakaji,
iii. Ulevi na matumizi ya dawa za kulevya kama vile bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika,
iv. Kupiga au kupigana,
v. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma,
vi. Utoro wa aina yoyote pamoja na kutokuhudhuria masomo bila sababu,
vii. Kudharau bendera ya Taifa na Wimbo wa Taifa,

viii. Kuwa na mimba,

ix. Kuoa au kuolewa,

x. Kutoa mimba,

xi. Kugoma, kuchochea na kungoza au kushiriki kuvuruga amani,

xii. Kukataa adhabu kwa makusudi,

xiii. Kupatikana na makosa ya jinai, na

**xiv. Kuwa na simu ya mkononi (mwanafunzi atatumia simu ya shule).**

### 4.2 MAMBO YA KUZINGATIA SHULENI

i) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule ni muhimu,
ii) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine atakazopewa,
iii) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo shule hii,
iv) Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule,
v) Kuvaa sare ya shule wakati wote awapo shuleni na nje ya shule na anapokuwa kwenye shughuli za kitaaluma,
vi) Kuzingatia ratiba ya Shule wakati wote,
vii) Sare za shule huvaliwa wakati wote ukiwa shuleni, wakati wa Kwenda nyumbani ,na wakati wa kurudi shuleni,
viii) Lugha ya mawasiliano awapo shuleni kwa muda wote ni **kiingereza,**
ix) Mwanafunzi awe na bidii ya kujielimisha na kufanya mazoezi na majaribio yote darasani na mitihani yote ikiwemo ya nje,
x) Kila mwanafunzi atawajibika kulinda na kutunza mali ya shule na yake binafsi, kwa Mwanafunzi atakaye haribu mali ya shule atapaswa kulipa mara moja baada ya kuthibitika,
xi) Kila mwanafunzi analazimika kuwa na nidhamu ya hali ya juu katika Maongezi na walezi wake pasipo kutumia lugha chafu,
xii) Ruhusa ya kulala nje ya shule itatolewa na makamu mkuu wa shule baada ya kupelekwa maombi kwa kupitia kwa mlezi wa nyumba na mwalimu wa zamu anayehusika,
xiii) Ni kosa kwa mwanafunzi kwenda nje ya mipaka ya shule bila ruhusa. Ruhusa ya kutoka nje ya eneo la shule ni lazima ipatikane kutoka kwa mwalimu wa zamu ambaye atatoa karatasi maalumu ya ruhusa.

xiv) Mwanafunzi aliyeruhusiwa kwenda nje ya mipaka ya shule lazima avae sare ya shule,
xv) Wanafunzi hawaruhusiwi kutembelea sehemu zifuatazo:-
(i) Vilabu vya pombe

(ii) Nyumba za starehe kama dansi,filamu au video n.k

(iii)Nyumba za kulala wageni.

xvi) Wanafunzi wasitembelee sehemu zifuatazo isipokuwa kwa kibali maalum:-
(a) Ofisi ya walimu,
(b) Ofisi za shule/utawala,
(c) Nyumba za watumishi wote wa shule.

### 4.3 AHADI ZA SHULE

**AHADI NA UTII WA SHERIA NA TARATIBU ZA SHULE.**

Mimi ______________________________________________________________

Naahidi kwamba nitafuata na kutii kwa muda wote nitakaokuwa ninasoma hapa shuleni kanuni na sheria za Shule.

Sahii________________ Tarehe. ……………………

## 5.0. MAAGIZO MENGINE

### 5.1 FEDHA ZA MATIBABU

Gharama zote za matibabu zitagharimiwa na mzazi/mlezi. Hivyo mzazi/mlezi ampe mwanae pesa ya kutosha ya matibabu au amkatie bima ya afya.

### 5.2 **VYETI BANDIA VYA HOSPITALI**

Baadhi ya wazazi hushirikiana na watoto wao kutafuta taarifa bandia ili wasifanye kazi za shule au kula vyakula aina fulani, mzazi au mototo asifanye hivyo kwa kuwa mazingira hayatamfaa kujifunza.

### 5.3 FEDHA YA MATUMIZI

Mwanafunzi haruhusiwi kwenda mjini. Mzazi ahakikishe anamnunulia mtoto wake mahitaji mhimu, pia ampe fedha ya kutosha kwa ajili ya matumizi shuleni)

## 6.0 MICHANGO MBALIMBALI

| Na | Aina ya mchango | kiasi |
|---|---|---|
| 1 | Mchango wa uendeshaji wa shule | 65,000/= |
| 2 | Tahadhari | 5,000/= |
| 3 | Nembo | 5,000/= |
| 4 | Kitambulisho cha shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

Michango ya uendeshaji wa shule,tahadhali, nembo, na kitambulisho cha shule ilipwe kupitia akaunti ya benki; **NMB 52110010326 YENYE JINA KAKONKO GIRLS SECONDARY SCHOOL**

**7.0 MWISHO:**

Gharama zote za kwenda nyumbani na kurudi Shuleni ni juu ya Mzazi/ Mlezi

______________________ _____________________

Sahihi ya Mwanafunzi Sahihi ya Mzazi/Mlezi

Tarehe: ____________________ Tarehe: ________________

Namba ya simu ya Mzazi/Mlezi________________________________________________

**UTHIBITISHO WA MWANAFUNZI; -**

Nathibitisa kuwa maelezo niliyoandika katika fomu hii ni sahihi.

Jina_______________________ Sahihi___________ Tarehe ……………………………..

KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA KAKONKO.

ISDORA ROGATH MROSO.

**MKUU WA SHULE**

**HISTORIA YA MWANAFUNZI**

1. Jina la Mwanafunzi……………………………...............................................
2. Tarehe ya kuzaliwa..............................................................................................
3. jina la Baba……………………………………………………………………………..
4. Jina la Mama…………………………………………………………………………...
5. Jina kamili la Mlezi…………………………………………………………………….
6. Anuani ya Mzazi/Mlezi………………………………………………………………...
7. Uhusiano wa Mlezi…………………………………………………………………….
8. Kazi ya Baba (Mkulima,Mfanyabiashara, Mfanyakazi ( kata isiyo husika).

11. Kama ni Mfanyakazi, kazi yake ni……………………………………………………
12. Afya ya Mwanafunzi, kama anayo matatizo ya kiafya na hivyo hustahili huduma maalumu, Tafadhari Mzazi/Mlezi aeleze wazi

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………

**Ndugu wa Karibu:-**
**Jina kamili ,kazi yake, anuani yake(simu)**

1………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………..

2………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………..

3………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………….

4………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………..

**MEDICAL EXAMINATION FORM**

Student's names…………………………………………………………………………………………….

Age……………………………………………………………………………………………………………

Stool test…………………………………………………………………………………………………..

Blood group………………………………………………………………………………………………

Urine analysis……………………………………………………………………………………………

Syphilis test………………………………………………………………………………………………

Chest test…………………………………………………………………………………………………

Speech test………………………………………………………………………………………………

Eye test……………………………………………………………………………………………………

Abdomen test……………………………………………………………………………………………..

Additional information and physical defect or impairment to pursue further education

……………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………

Name……………………………………………………………………………………………………….

Signed……………………………………………………………………………………………………...

Designation……………………………………………………………………………………………..

Official stamp

Date……….................................................